

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA**

**24 JUNI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA– TAREHE 24 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

445. **MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la kubebea Wagonjwa katika Wilaya ya Simanjiro.

446. **MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Hospitali ya Halmashauri ya Bunda DC na Kituo cha Afya Mugeta vitafunguliwa.

**WIZARA YA MAJI:**

**447. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku ya ukarabati wa miradi ya maji kama inavyofanya kwa miradi ya barabara.



**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**448. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini barabara ya kwenda Makumbusho ya Mkwawa itajengwa kwa kiwango cha lami na kukarabati jengo la Chifu Adam Sapi Mkwawa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **449. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Ifakara Kibaoni hadi Mahenge Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **450. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Polisi Mtwara.



**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**451. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini uwepo wa Wakalimani wa lugha ya  
alama kwa vipindi vya habari vya televisheni, na  
ziara za Viongozi utakuwa wa lazima.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**452. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS  
(KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na  
Mipango:-

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu uuzaji na  
ununuzi fedha za kigeni kwa kulipa kima tofauti  
kwa USD 100, USD 20, USD 10 na USD 5.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**453. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA  
(CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, Zanzibar wameshirikishwaje kuandaa  
Mtaala wa somo la Historia ikizingatiwa historia  
ya Zanzibar na Bara ipo tofauti.

**WIZARA YA AFYA:**

**454. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO  
MWAKAMO (KIBAHA VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha  
kitengo cha kutibu Wagonjwa wa Afya ya Akili  
kwenye kila Hospitali za Halmashauri nchini.

### III. HOJA ZA SERIKALI:

#### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***(Majadiliano yanaendelea)***

### IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa kwa Hatua zake zote)***

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2022 (*The Appropriation Bill, 2022*).

**DODOMA  
24 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**